

MlokoleBinti



**MUNGU ATAKUPA
MUME WA HADHI YAKO
USITAKE VIKUBWA!**

www.mlokolebinti.com

WEZESHA HUDUMA



@mlokolebinti



0713300038

MUNGU ATAKUPA MUME WA HADHI YAKO USITAKE VIKUBWA.

Mwanzo 2:18

BWANA Mungu akasema,Sivema huyo mtu awe peke yake,nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye.

Hapa kwenye kufanana hapaaa!Hutaki wa kufanana nae uchumi? Ila mfanane ucha Mungu! yaani unakuta mtu mwaka mzima anakataa wanaume kwa sababu ndogo-ndogo (Very Minor Issues), anataka Fairy Tale hakika Tamthilia zimewaharibu,na uhalisia ni kwamba *Mungu atakupa Mume lakini sio hio fairy tale type of love!*.

Mpendwa haya mambo wafanye vijana wenye umri wa miaka 23-25! hawa bado wana kamuda! na Kwa upande wangu hawa nawakubaliaga kuwa inawezekana kwani Muda bado wanao mkononi!, Let them explore all options! Acha wavunje mifupa kwani meno yanaruhusu kwa upande wao.

Sasa unakuta Mtu mzima miaka 28 kwenda juu, ANA MTOTO JUU! Ambaye ashapigwa tukio na Baby Dady kwa hizo-hizo *Fairy Tale* zake naye bado analeta swaggz za KUNTAKA MWANAUME WA AINA FLANI! Hapa Swalii la Kujiuliza ni Je, Hiyo aina ya wanaume unayotaka wao wanakutaka??? Tuwe tu Wakweli?, Na Ukweli ni kwamba HAWAKUTAKI MWANANGU NDIYO MAANA AGE GO AND IS GOING VERY FAR!

Tutumia tu akili ya kawaida (*Common-Sense*) mwanaume mwenye hela zake katika hali ya kawaida ana supply kubwa ya wanawake, Sasa ataanzaje kukutaka wewe mwenzetu hata Mia Hunaa???

Mnapenda kwenda vina virefu afu mkizama mnaanza kumlaumu Mungu!, Wewe unaona mtu hufanani nae kwanini unajizima data ? Unaishia kutafunwaaa na kuachwa!, Unataka mwanaume mwenye Gari ilihali kila wakati wewe ni mtu wa ku request! Unataka mwanaume awe na career ?? Je,Wewe unayo hio career?

YOU CAN GET THESE MEN IF YOU WORK REALY HARD TO CHANGE YOUR STATUS UENDANE NAO!, NA HAPA KUWAPATA INAKUWA RAHISI HIVYO THE TIME YOU WANT THEM, YOU FIND YOURSELF THEY WANT YOU TOO NA MAMBO YANAKUWA MAMBO BAM BAM! Otherwise tafuta wa kufanana na wewe mwanangu!, Ligi kubwa waacie wakubwa zako!.

Mungu alisema atakupa mtu wa kufanana na wewe lakini sio TAMTHILIA !, Angalia Dada zako je, Wame wapata wanaume wa hizo tamthilia ? Thubutuuu! ,Usiharibu maisha yako kwa kukosa maarifa madogo yaani Mtu anakwambia hana mtu mwaka mzima amekataaa watu SIO chini ya 10 na anakwambia mwenyewe sababu hasa ni hawana hela na hawana maisha anayo-yataka! , Mpendwa katika hili tunaanza na WEWE una maisha gani?, Yaani huna mbele wala nyuma!, JUST A BROKE GIRL WITH DANGEROUS AMBITIONS!, If you are young and beautiful maliza geji dada.

Haya mambo ya kukataaa wachumba sio mazuri, Jitahidi jua linazama kuweza KUJITAFAKARI! na kuangalia upande wa pili wa shilingi ya kwamba MAYBE AINA HIYO YA WANAUME HAIPo? NA KAMA IPO MAYBE SIO KWA AINA YAKO YA WANAWAKE!

Enzi zetu mnaambiwa Someni mpate Mabwana wa ofisini!, Na kipindi hicho mnawakuta Wasomi wanataka Wasomi wenzao!, Sasa jifanyeni mapana stini mje muokoteze hawa Choka mbaya! SIO Msome mkomboe fikraaa! hili Hapana! Bali ni Someni mpate Mabwana wa Maana, School in the head na nyinyi kidogo school in the head mambo yana-balance! *MPENDWA LIKE POLES ATTRACT UNLIKE POLES REPEL!*.

Katika Drama zako hizo Mpendwa uko peke yako, Fanya kuzihesabu MBINGU out!, Mwendo ni kupewa wa kufanana naye!, Mki-oana mta-tafuta njia wote! Si una-oná wazazi wetu! Wanaanza kulala chini mpaka nyumba wana jenga! basi wewe ungekuwa mama kwa mfano, ungemkataa Baba yako kwa sababu hana-kitu bila kujali riziki anagawa Mungu peke yake!, MNAO KATAA WANAUME BILA SABABU ZA MSINGI MJITAFAKARI!, WAUME WOTE WAPO DUNIANI TAYARI MUNGU HATASHUSHA MALAIKA KUJA KUKUOA! WATU WOTE WA MUNGU, MASKINI WA KWAKE NA TAJIRI WA KWAKE!.

www.mlokolebinti.com